Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

# ELIMU Bulletin

JARIDA LA MTANDAONI: Toleo Na.40 - 2024

wizara_elimuTanzania wizara_elimuTz www.facebook/moestvt.com www.wyestu.blogspot.com www.moe.go.tz ELIMUTZ

*Tunaboresha Elimu Yetu*




## Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la 2023

# Sasa Rasmi



# Rais Samia kuzindua Sera ya Elimu na Mitaala

## - KAZI IENDELEE -




**BODI YA UHARIRI**

Sylvia Lupembe
***Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini***

**Wachangiaji:**
Oliva Kato
Elizabeth Pancras
Veronica Chitunda
Nazareth Mwakabuta

**Mawasiliano:**
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
Mji wa Serikali Mtumba, Mtaa wa Afya - Dodoma
S.L.P. 10, 40479 DODOMA.
Simu: +255 26 296 3533

**Jarida hili linatolewa na**
Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

# TAHARIRI

## WATAFITI WA NDANI WASIPUUZWE, TAFITI ZAO ZIPEWE KIPAUMBELE

Katika muktadha wa maendeleo ya kitaifa, watafiti wa ndani wanachukua nafasi muhimu sana katika kuchochea maendeleo, kwani kujitolea kwao katika utafiti, ubunifu na uvumbuzi kunaleta matokeo chanya katika nyanja za kijamii na kiuchumi.

Ikumbukwe kwamba watafiti hao wana uelewa wa kutosha juu ya changamoto zinazokabili mazingira yao ya ndani, hali hii inawawezesha kutatua changamoto hizo kwa njia bora zaidi ikilinganishwa na watafiti wa nje, hatua hiyo inajenga heshima na utambulisho kwa Taifa.

Akizungumza katika kilele cha Maonesho na Kongamano la Tisa la Sayansi, Teknolojia na Ubunifu Disemba 02, 2024 jijini Dar es Salaam, Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Doto Biteko alisisitiza jamii ya Kitanzania kutambua na kuthamini tafiti za wanasayansi wa ndani ya nchi ili kutatua changamoto zilizopo.

Katika kuweka msisitizo Kiongozi huyo alitoa wito wa kutumia kikamilifu tafiti za wanasayansi wa ndani badala ya kuwavunja moyo, na kuwapa fursa zaidi ili waendelee kutafiti kwa maendeleo ya nchi.

Ingawa ni muhimu kuwapa kipaumbele watafiti wa ndani, suala la ushirikiano wa kimataifa bado linahitajika. Hata hivyo tunaamini kwamba watafiti wa ndani anapokuwa na nguvu na uwezo, wanaweza kushiriki kwa usawa zaidi na kuchangia kwa kiwango kikubwa katika miradi ya kitaifa na kimataifa.

Ni jukumu letu kuhakikisha kwamba watafiti wa ndani wanapata msaada na fursa zinazohitajika ili waweze kutoa mchango wao muhimu katika jamii na taifa kwa ujumla.







Uzinduzi Sera ya Elimu >

# Rais Samia kuzindua Sera ya Elimu, Mitaala




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kuzindua Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, Toleo la 2023 na Mitaala Iliyoboreshwa Januari 31,2025 Jijini Dodoma.

Akizungumza na waandishi wa habari Januari 10, 2025 Jijini Dodoma, Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda amesema kuwa uzinduzi wa Sera hiyo ni hatua muhimu katika kuchochea mageuzi makubwa katika sekta ya elimu nchini, yakigusa elimu ya awali hadi kidato cha sita.

Aidha Waziri Mkenda ameongeza kuwa Serikali imezingatia michango na hoja mbalimbali kutoka kwa wananchi kuhusu sera hiyo, na imejumuisha majibu ya maswali mengi katika sera na mitaala mipya.

"Hivi sasa tunayo mitaala mipya ambayo tunaitekeleza kwa awamu na suala hili ni kubwa na mageuzi yaliyopo kwenye sera ni makubwa sana," Prof. Mkenda.

Amesema mabadiliko hayo yataenda kugusa vizazi na vizazi kwani ukamilifu wa utekelezaji wake ni kuanzia elimu ya awali mpaka kidato cha Sita licha ya kuwa utachukua muda kwasababu walianza hatua kwa hatua na kuongeza kuwa yataenda kuleta muelekeo ambao utabadilisha taswira ya elimu nchini.

Prof. Mkenda amesema Serikali inasikia michango na hoja mbalimbali zinazotolewa na watu kuhusu Sera ya Elimu hivyo inaendelea kufuatilia ila majibu ya hoja zote zinazotolewa ziwepo ndani ya Sera hiyo.

"Mfano mjadala mkubwa unaoendelea kwa sasa nchini ni kuhusu somo la Kingereza, ukienda kwenye sera utaona suala la lugha, ukienda kwenye mitaala utakuta ufundishaji wa lugha, tunasikia watu wanazungumza suala la akili mnemba ni suala kubwa sana. Alibainisha Waziri huyo.

# Matumizi Sayansi, Teknolojia na Ubunifu >




## Serikali kuendelea kuimarisha matumizi ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu - Dkt. Biteko

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dkt. Doto Biteko amesema kuwa Serikali itaendelea kuimarisha matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu hususan kwenye eneo la utafiti ili kutatua changamoto za kiuchumi na za kijamii nchini.

Dkt. Biteko ameeleza hayo Disemba 02, 2024 jijini Dar es Salaam wakati akifungua Kongamano na Maonesho ya Tisa ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu, ambapo amesisitiza kuwa ni muhimu kutambua, kuthamini na kutumia tafiti za wanasayansi wa ndani ili kuendelea kuwatia moyo kwa maendeleo ya Taifa.

"Tutumie tafiti za wanasayansi wa ndani badala ya kuwavunja moyo na kila anayejaribu kwa kutafiti apewe fursa ili aendelee kutafiti zaidi na matokeo tutayaona," amesema DKt. Biteko.

Ameongeza kuwa tangu mwaka 2015 Serikali imeshapokea kiasi cha shilingi bilioni 222.8 kwa ajili ya kujenga uwezo kwa wanasayansi wabunifu wakiwemo wanasayansi vijana, ili kuendeleza miradi mbalimbali.

Nae Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Prof. Adolf Mkenda amesema kwa kutambua jitihada za Wanasayansi na Watafiti wa ndani ya nchi, baadhi yao wametunukiwa vyeti kwa kutambua mchango wao kwa maendeleo yaliyofikiwa katika sekta mbalimbali ikiwemo Afya, Kilimo na Uvuvi.

Serikali kupitia Wizara imeanzisha Mfuko wa Mikopo nafuu ya Ubiasharishaji Bunifu Tanzania utakaojulikana kwa Jina la *Samia Fund*, ambao umepata fedha kutoka kwenye Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET).

Amesema kuwa ili kuwasaidia watafiti watakaojikita katika kufanya tafiti za mabadiliko ya Tabianchi Serikali ya watu wa Norway imetoa ufadhili wa shilingi Bilioni 6.3 kuwasaidia watafiti 19.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Utamaduni, Michezo na Sanaa Mhe. Husna Sekiboko ameipongeza serikali kwa kuanzisha mfuko wa kuwasaidia wabunifu na kuahidi kuweka msukumo kuhakikisha mfuko huo unaongezewa fedha ili kuwezesha bunifu na tafiti zinakwenda kuleta tija katika taifa.

Elimu kwa kila Mtanzania>

# Wanafunzi wa kike 12,000 nchini walokatiza masomo kurudi shuleni



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda amesema Serikali imedhamiria kuwarudisha shule Wasichana 12,000 walikatisha masomo kutokana na sababu mbalimbali.

Waziri Mkenda ameeleza hayo Januari 13, 2025 mkoani Morogoro, akizindua Warsha ya Tathmini ya Utekelezaji wa Mradi wa SEQUIP AEP, ambapo ameipongeza Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima kwa kutekeleza kwa ufanisi jukumu la kuimarisha utolewaji wa Programu ya Elimu ya Sekondari kwa njia Mbadala kwa wasichana waliokatisha masomo.

Mkenda ameeleza kuwa mradi wa SEQUIP umeleta mapinduzi makubwa katika elimu ya sekondari, na kwamba Mradi huo wa thamani ya dola za Kimarekani milioni 500 unalenga kuboresha miundombinu ya elimu na kutoa mafunzo kwa walimu zaidi ya 29,300 wanaofundisha masomo ya Sayansi na Hisabati na kusaidia ujenzi wa shule mpya 830.

"Tunaendelea kutekeleza Sera mpya ya Elimu ambapo kuanzia 2027 elimu ya lazima itakuwa miaka 10. Pamoja na miradi mingine, tunaendelea kuandaa miundombinu bora kuwezesha utolewaji wa elimu," alisema Waziri Mkenda.

Mkuu wa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima Prof. Michael Ng'umbi ameishukuru Serikali kwa kuendelea kuiamini na kuiwezesha kutekeleza Mradi wa SEQUIP - AEP, ameahidi kuwa Taasisi itaendelea kufanya kazi kwa weledi na kwa ufanisi ili malengo ya mradi yaweze kutimia.



Mafunzo ya TEHAMA>

# Mradi wa BOOST wawezesha mafunzo ya TEHAMA kwa walimu wa Awali na Msingi



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Dkt. Charles Mahera amesema maendeleo ya sayansi na teknlojia yamechagiza uhitaji wa matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji kwa ajili ya kurahisisha utoaji elimu nchini.

Dkt. Mahera ameyasema hayo Disemba 18, 2024, katika ufunguzi wa mafunzo ya matumizi bora na salama ya vifaa vya TEHAMA na stadi za kidigitali kwa walimu wa Awali na Msingi yanayotekelezwa kupitia Mradi wa Kuimarisha na Kuendeleza Elimu ya Awali na Msingi (BOOST).

"Kwa mwaka huu Serikali kupitia Mradi wa BOOST itanunua na kuweka vifaa vya TEHAMA katika Vituo vya Walimu na shule teule 600 zilizobaki ili kukamilisha vituo vya walimu na shule teule 800 vilivyopangwa katika kipindi chote cha utekelezaji wa mradi" alisema Mahera.

Sambamba na hilo amesema mradi huo umetoa mafunzo kwa Maafisa Elimu Kata, Walimu Wakuu na Walimu wa TEHAMA kutoka katika Vituo hivyo 200 na imepanga kutoa mafunzo kwa washiriki 1,800 kutoka katika Mikoa yote na Halmashauri zote Tanzania Bara.

Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Lina Rujweka amesema TEHAMA ni mojawapo ya fani zilizowekewa msisitizo kufundishwa katika shule za sekondari mkondo wa Amali. Hivyo ni vema kuanza kuandaa wanafunzi ngazi ya elimu ya awali na msingi kupata stadi za TEHAMA.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Uthibiti Ubora wa shule Mwl. Ephraim Simbeye amesema Serikali inaendelea na jitihada mbalimbali za mageuzi makubwa katika sekta ya elimu, ili kuandaa wahitimu wenye maarifa na ujuzi utakao wawezesha kujitegemea, kujiajiri na kuajiriwa.



Uchumi wa Buluu >



# Rais Mwinyi: Sayansi ya Bahari nguzo ya Uchumi waBuluu

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi amesema kuimarika kwa Taasisi ya Sayansi za Bahari ya Chuo Kikuu Cha Dar-Es- Salaam, kutasaidia kutoa matokeo ya tafiti mbalimbali za uchumi wa buluu ambazo zitatumika kutengeneza sera bora zitakazoendana na tafiti hizo ili kukuza sekta ya uchumi wa buluu.

Rais Mwinyi ameseama hayo Januari 05, 2025 Visiwani Zanziba akizungumza baada ya kuweka jiwe la msingi la Jengo la Taaluma na Utawala la Taasisi ya Sayansi ya Bahari, Buyu, akisisitiza kuwa taasisi hiyo itasaidia kuendeleza uchumi wa bluu kupitia tafiti na mafunzo ya wataalamu wa sekta za uvuvi, utalii, na mazao ya baharini.



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Prof. Adolf Mkenda, amempongeza Rais Mwinyi kwa juhudi kubwa katika kuimarisha sekta ya elimu, akisisitiza kuwa mageuzi hayo ni msingi wa maendeleo endelevu ya taifa.

Prof. Mkenda ameongeza kuwa Jengo la Taasisi ya Sayansi ya Bahari, Buyu, linajengwa na Serikali kupitia Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET) ambao unatekelezwa na Wizara ukilenga katika kuongeza Fursa za Elimu ya Juu nchini na kuchagiza maendeleo ya kiuchumi

Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete amesema uwekaji jiwe la msingi katika Taasisi hiyo unaashiria hatua muhimu katika kuendeleza miundombinu ya elimu na ubora wa kitaaluma katika Chuo hicho ili kuendeleza mipango na sera za uchumi wa bluu.

Nae Makamu Mkuu wa Chuo hicho Prof. William Anangisye amesema mradi huo wa zaidi ya Shilingi bilioni 11 unaofadhiliwa na Benki ya Dunia unahusisha ujenzi wa maabara 5, madarasa yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 300, majengo ya utawala pamoja na ukumbi wa kisasa.

Teknolojia katika Ujifunzaji >

# Sera mpya ya Elimu imezingatia matumizi ya Teknolojia katika ujifunzaji - Prof Nombo



Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Carolyne Nombo amesema Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023, imezingatia na kusisitiza matumizi ya teknolojia za kidijitali katika sekta ya elimu ili kurahisisha ujifunzaji na ufundishaji.

Aidha, pamoja na masuala mengine, amesisitiza dhamira ya Serikali katika kujenga uwezo na kuzalisha walimu mahiri kwenye matumizi ya teknolojia za kidijitali.

Prof. Nombo ameeleza hayo Januari 08, 2025 jijini Dodoma akizungumza na Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Maendeleo la Ubelgiji-ENABEL, Bw. Koenaraad Goekint, juu ya mradi unaotekelezwa na Shirika hilo nchini kwa lengo la kujenga uwezo na kuimarisha mazingira ya utoaji wa elimu kidigitali.

"Utoaji wa elimu kidijitali ni kipaumbele chetu, vipaumbele vyenu na mradi mnaotekeleza unasadifu malengo yetu yanayodhamiria kuwezesha ujuzi wa teknolojia za kidijitali kwa vijana na walimu" alisema Prof. Nombo.

Goekint amesema Shirika hilo limejitolea, pamoja na maeneo mengine, kuimarisha utoaji wa elimu jumuishi kama nyenzo ya kufikia uchumi endelevu.

Aidha, Goekint alifafanua kwamba mradi wa elimu ya ubunifu wa dijitali utaimarisha uwezo wa kufundisha stadi za kidigitali.

Mkurugenzi wa Idara ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu, Prof. Ladslaus Mnyone amesema kuwa teknolojia za kidijitali ni nyenzo muhimu katika kuharakisha mageuzi kwenye sekta ya elimu na sekta nyingine, hivyo kupitia utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa masuala hayo, Serikali imedhamiria kuimarisha mazingira ya kujifunzia na kufundishia stadi za kidijitali hususan kwa watoto na vijana.



## Umahiri Sekta ya Teknolojia >



# DIT yapongezwa kutoa wahitimu mahiri Sekta ya Teknolojia ya utengenezaji bidhaa za ngozi



Naibu Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia Mhe. Omari Kipanga ameipongeza Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) kwa kuendelea kutoa elimu bora na wahitimu mahiri wenye uwezo wa kutatua changamoto mbalimbali za kijamii kupitia ujuzi wanaoupata wakiwa mafunzoni.

Mhe. Kipanga ametoa pongezi hizo Disemba 13, 2024 katika Mahafali ya Kumi na Nane Duru ya pili katika kampasi ya DIT Mwanza, ambapo amesema kuwa Serikali inajivunia maboresho yanaofanyika katika sekta ya elimu yanayowezesha kuzalisha wataalam wanaoajirika, kujiajiri na kutengeneza ajira kwa wengine.

Nae Mwenyekiti wa Baraza la Taasisi la Taasisi hiyo Mhandisi Dkt. Richard Masika, ameipongeza serikali kwa namna inavyoboresha miundombinu katika sekta ya elimu, na ameishukuru kwa kuanzisha kituo cha ujasiriamali, ubunifu, uhaulishaji wa teknolojia pamoja na malezi ya kampuni kwa Taasisi ya DIT.

Mafunzo SEQUIP >

# Walimu wa Sekondari 40,000 kunufaika na mafunzo kupitia mradi wa SEQUIP



Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Dkt. Charles Mahera, amesema kuwa serikali imejipanga kikamilifu kuhakikisha kuwa elimu ya sekondari inaimarishwa kwa walimu na wanafunzi.

Dkt. Mahera amesema hayo Januari 06, 2025 mkoani Mara wakati akifungua mafunzo ya siku tano kwa walimu kutoka mkoa wa Simiyu na Mara, mafunzo hayo yanalenga kuimarisha mbinu za kisasa za kufundishia ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia na mahitaji ya soko la ajira.

Dkt. Mahera amesema mafunzo hayo yanafadhiliwa na Mradi wa Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Sekondari (SEQUIP) na yanalenga kuwafikia walimu 40,000 ifikapo 2026, ambapo walimu 29,328 tayari wamenufaika na mafunzo hayo.



"Mafunzo haya yamekuwa na mchango mkubwa katika kuhakikisha walimu wanakuwa wabunifu, wanajiamini, na wana uwezo wa kufundisha masomo yenye changamoto kama sayansi na hisabati," alisema Dkt. Mahera.

Akizungumza Mratibu wa Mradi wa SEQUIP Dkt. Nicholaus Gati, ameeleza kuwa mradi umefanikiwa kwa asilimia 85, ukilenga kuwapa wanafunzi wa kike fursa zaidi kushiriki kikamilifu katika elimu ya sekondari.

Naye Mkurugenzi wa Ualimu kutoka Wizara ya Elimu ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Dkt. Huruma Mageni amesisitiza kuwa mbinu za kisasa zinazotolewa katika mafunzo hayo zinasaidia kukuza ubunifu wa walimu na ufanisi wa wanafunzi.

Wakizungumza kuhusu mafunzo hayo Mthibiti Mkuu Ubora wa Shule kutoka Halmashauri ya Mji wa Bunda Mwl. Paulina Makolo pamoja na Mwalimu Eliud Myovela kutoka Shule ya Sekondari Tarime wameishukuru Serikali kwa kuwapatia kipaumbe cha mafunzo hayo ambayo yatawaongezea ufanisi katika ufundishaji na matumizi ya TEHAMA.

Ustawi wa Uchumi >

# Taifa haliwezi kustawi kiuchumi bila mafundi sanifu, wanasayansi



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Daniel Mushi, amesema Serikali inathamini mchango mkubwa wa wanasayansi, wahandisi, watafiti na wabunifu katika kufikia azma ya kuwa nchi ya uchumi wa viwanda.

Prof. Mushi ametoa kauli hiyo leo Disemba 06, 2024 jijini Dar es Salaam akihutubia katika mahafali ya 18 ya Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) ambapo amewasisitiza Wahitimu kutumia kikamilifu elimu waliyoipata kwa maendeleo yao binafsi na taifa kwa ujumla.

Ameeleza kuwa Serikali imeendelea kuongeza fursa za mafunzo na kwamba katika mwaka wa fedha 2023/2024, iliongeza udahili katika Vyuo vya Elimu ya Ufundi kutoka wanafunzi 171,581 hadi wanafunzi 235,804 pamoja na kuendelea kutoa mafunzo kwa wakufunzi kuwajengea uwezo wa ufundishaji wa mitaala inayoendana na mabadiliko ya teknolojia na mahitaji ya soko la ajira.

Mwenyekiti wa Baraza la Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) Mhandisi Dkt. Richard Masika ameishukuru Serikali kwa kuipatia Taasisi hiyo fedha kutekeleza miradi ya maendeleo, na kwamba inajivunia kutekeleza Mradi wa Kujenga Ujuzi na Ushirikiano Afrika Mashariki (EASTRIP) ambao unawezesha ujenzi wa miundombinu ikiwemo Kituo cha Kikanda cha Umahiri wa TEHAMA (RAFIC) katika Kampasi Kuu ya Dar es Salaam.

"Wizara pia imetupatia mkopo wa riba nafuu kutoka serikali ya Italia ambapo sehemu ya fedha hizo inalenga kuanzisha kituo cha ujasiriamali, ubunifu, uhaulishaji wa teknolojia, hatua hii inatuwezesha kuendelea kuunda, kuendeleza na kulea teknolojia mbalimbali" alieeleza Dkt. Masika.



# Anuani za Taasisi zilizo chini ya Wizara

Katibu Mtendaji,
**Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU),**
Jengo la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
S.L.P 6562,
7 Mtaa wa Magogoni,
11479 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2113694, 2113691
Barua Pepe: es@tcu.go.tz

Mkurugenzi Mtendaji,
**Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB),**
HESLB House, 1 Mtaa wa Kilimo -TAZARA,
Barabara ya Mandela,
P.O. Box 76068,
15471 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 736 665 533/ 739 665 533
Baruapepe: ed@heslb.go.tz

Katibu mtendaji,
**Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA),**
Eneo la Viwanda Mikocheni,
Barabara ya Bagamoyo,
S.L.P 2624 au 32019,
14112 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2700493-6/9 na 22 2772423
Barua Pepe: esnecta@necta.go.tz

Mtendaji Mkuu,
**Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTVET),**
S.L.P 17007, DODOMA.
Simu: +255 26 2323 121 / 0733 77 77 51
Barua Pepe: info@nacte.go.tz

Mtendaji Mkuu,
**Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM),**
Nunge Street, Old Catholic Church Road,
S.L.P 71, BAGAMOYO, PWANI.
Simu: +255 23 244 0216
Barua Pepe: adem@adem.ac.tz

Mkurugenzi Mkuu,
**Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH),**
Barabara ya Ali Hassan Mwinyi,
S.L.P. 4302,
14113 Kijitonyama,
DAR ES SALAAM.
Simu: +255 (022) 2771358/ 2774023/ 2700749
Baruapepe: dg@costech.or.tz

Mkurugenzi Mkuu,
**Taasisi ya Elimu Tanzania (TET),**
Plot 132, Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P. 35094, DAR ES SALAAM.
Simu: +255 0735 041168
Barua Pepe: director.general@tie.go.tz

Mkurugenzi Mkuu,
**Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA),**
S.L.P 34578,
Mikocheni B, Bima Road,
DAR ES SALAAM.
Simu:
Barua Pepe: info@tea.or.tz
dg@tea.or.tz

Mkurugenzi Mkuu
**VETA Makao Makuu,**
Plot No. 18, Central Business Park (CBP)
Barabara ya VETA,
S.L.P 802,
26 DODOMA.
Simu: +255 26 2963661
Baruapepe: info@veta.go.tz

Mtendaji Mkuu,
**Tume ya nguvu za Atomic Tanzania (TAEC)**
S.L.P 743,
23114 Engutoto, Block J, Plot No 216,
ARUSHA
Simu: +255 272 9700054
Barua Pepe:dg@taec.go.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM),**
Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere Mlimani,
S.L.P. 35091, Mtaa wa Chuo Kikuu
16103 Dar es Salaam
Simu: +255222410700
Baruapepe: vc@udsm.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Ardhi University (ARU),**
Plot No. 3, Observation Hill Blok L,
University Road,
P.O. Box 35176, DAR ES SALAAM.
Simu: +255 738 357 310-12
Baruapepe: aru@aru.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi, Muhimbili (MUHAS),**
9 Barabara ya Umoja wa Mataifa,
Upanga Magharibi,
S.L.P. 65001,
11103 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2150302-6
Baruapepe: vc@muhas.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA),**
S.L.P 3000,
Barabara ya Edward Moringe, Mtaa wa Kilimo,
01 MOROGORO
Simu: +255 23 260511-4
Barua Pepe: sua@sua.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Mzumbe (MU),**
S.L.P 1, MOROGORO
Simu:
Barua Pepe: mu@mzumbe.ac.tz
info@mzumbe.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM),**
S.L.P 259,
Mtaa wa Benjamin Mkapa,
Jengo la Benjamin Mkapa,
41107 DODOMA.
Simu: +255 26 2310001/2/3
Barua Pepe: vc@udom.ac.tz
relations@udom.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Huria Tanzania (OUT),**
S.L.P. 23409,
14110 Open University Road,
Kinondoni Municipality,
DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2668820/ 2668992
Baruapepe: vc@out.ac.tz

RASI wa Chuo,
**Chuo Kikuu kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE),**
Taifa Road Next to Benjamin Willium,
S.L.P 2329,
15105 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2850975
Barua Pepe: principal@duce.ac.tz
dpacademic@duce.ac.tz

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Ushirika Moshi,**
06 Barabara ya Sokoine Moshi,
S.L.P 474
KILIMANJARO
Simu: +255 272 751 833
Barua Pepe: info@mocu.ac.tz

Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kushiriki Cha Elimu Mkwawa (MUCE),**
Mtaa wa Mkwawa Chuo,
S.L.P. 2513,
51111 IRINGA CBD.
Simu: +255 26 2702 751
Baruapepe: principal@muce.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST),**
S.L.P. 131,
Barabara ya 01 MUST,
01 MBEYA.
Simu: +255(0)25 2957542/4
Barua pepe: vc@mustnet.

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NMIST),**
Kampasi ya Tengeru, Barabara ya Nelson Mandela,
S.L.P. 447,
23301 TENGERU, ARUSHA
Simu +255 272970001
Baruapepe: vc@nm-aist.ac.tz

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere,**
S.L.P 976, Butiama, MARA
Simu:
Barua Pepe: info@mjnuat.ac.tz

Mkurugenzi
**Bodi ya Huduma za Maktaba (TLSB),**
27 Mtaa wa Bibi Titi Mohamed,
S.L.P 9283
DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2150048/9
Barua Pepe: info@tlsb.go.tz

Katibu Mtendaji,
**Tume ya Taifa ya UNESCO,**
7 Magogoni Street,
P. O. Box 20384,
11479 DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2126598/ 22 2134292
Baruapepe: info@natcom.go.tz

Mkurugenzi,
**Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW)**
23 Mtaa wa Bibi Titi Mohammed,
S.L.P. 20679,
11103 DAR ES SALAAM
Simu:
Baruapepe: info@iae.ac.tz

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Ufundi Arusha (ATC),**
Junction of Moshi-Arusha and Nairobi Roads,
P.O. Box 296,
23105 ARUSHA.
Simu: +255 (0) 27-297 0056
Baruapepe: rector@atc.ac.tz/pro@atc.ac.tz

Mkurugenzi,
**Kituo cha Maendeleo Dakawa,**
S.L.P 1733,
MOROGORO.

Mkuu wa Chuo,
**Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT),**
Kona ya Bibi Titi na Barabara ya Morogoro
S.L.P 2958
11104 DAR ES SALAAM
Simu:
Barua Pepe: principal@dit.ac.tz

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA),**
30 Barabara ya Kibada,
S.L.P 9193,
17107 Kigamboni,
DAR ES SALAAM.
Simu:
Baruapepe: rector@mnma.ac.tz